# Siku ya kimataifa
# Ya watoto
# na vijana

• MAISHA MARA MOJA • DUNIA MOJA • MUNGU MOMOJA •

24 Aprili

2022

#IDCY22
#1Life1World1God

# Mawazo ya Mpango wa Mwisho wa Juma

## Ijumaa • Maisha

**Pendekezo la ratiba**

***Wimbo wa kiini***

Umeniumba kwa mikono yako, Bwana.
Nina maisha tele kupitia kwa pendo lako.
Siishi tena katika minyororo ya dhambi na mauti.
Waniweka huru, Bwana, Waniweka huru, Bwana,

Kuna uhuru katika wewe tuu.
Nina uzima wa milele katika wewe.

Twasherehekea na kucheza kulitukuza jina lako
Kwa ajili ya pendo lako la ajabu.
Hata katika dhoruba nitakuimbia wewe
Kwa ajili ya pendo lako la ajabu, Yesu!

Ninapojisikia kutengwa na kuachwa,
mikono yako ya upendo hunizunguka, Ninalindwa.
Nakufahamu wewe Mungu wangu, utanipenda siku zote
nami nakupenda, nami nakupenda.

## UTANGULIZI WA KIINI – MNENAJI WA 1 – MAISHA MARA MOJA – MIMI NI NANI?

[Kijana akiwa amevalia koti la rangi nzuri]

Habari, Mimi ni Yusufu, nina umri wa miaka 17.

Mimi mchunga kondoo pamoja na ndugu zangu. Kwa kweli, ni ndugu kwa mama mwingine.

[Akiongea kama kwa faragha, akinong'oneza] Nami humwambia baba yote wayafanyayo, ingawa sidhani wanapenda nifanye hivyo, hahaha. (anacheka lakini kwa woga)]

[Akinyooshea kidole koti] Hili koti langu, je unalipenda? Lilitengenezwa kwa ajili yangu na baba yangu, nafikiria ananipenda zaidi ya ndugu zangu. Najisia napendwa sana na baba yangu. [Anatabasamu] Yeye hunifanya nijisikie mimi mtu maalum.

Lakini kwa wakati huo huo, najisikia mpweke. Ndugu zangu hawanipendi; Hata hawataki kuzungumza nami.[Akionyesha kusikitika]

[Ukimya, kwa aibu analichukua koti lake]

Nachukia nyakati hizo. Unaona, wakati fulani nataka kuwa kama wao. Lakini upande mwingine, najua mimi ni wa pekee. Nina mahusiano na baba yangu yaliyo tofauti. Nami nina karama nyingine ambazo wao hawana. Unaona, nina ndoto hizi. Ndoto hizi huendelea kunijia. Siku moja niliwaambia juu ya ndoto moja niliyoiota, nao wakakasirika sana!

Huenda nikinyamaza tuu, nisiwaambie yale ninayoyafikiria au ninayoyaota, watanipenda zaidi kidogo. Upendo wa baba yangu ni mkubwa, lakini wakati fulani natamani ningependwa na ndugu zangu vile vile. Huenda siku zijazo. Unaweza kufikiria? Kuwa mtu ambaye wanamtamani? Hiyo itakuwa ndoto!

## KUTAFAKARI JUU YA KIFUNGU CHA BIBLIA



**NYENZO:**

- Biblia
- Taarifa  ya mapema
- Penseli

### Shughuli

Wape watoto na vijana vifungu hivi:

***'Mungu akaona kila kitu alichokifanya, na tazama, ni chema sana.'***

**(Mwanzo 1:31)**

***'Tusijisifu bure, tukichokozana na kuhusudiana.'***

**(Wagalatia 5:26)**

***'Nitakushukuru kwa kuwa nimeumbwa, kwa jinsi ya ajabu ya kutisha. Matendo yako ni ya ajabu, na nafsi yangu yajua sana.'***

**(Zaburi 139:14)**

Gawa taarifa ya mapema kwa watu wote. Kwenye kila karatasi wanatakiwa kuandika tafakari zao juu ya maswali

- Kuna kifungu, sentensi au neno linalojitokeza zaidi kwako? Taratibu anza kulirudia wewe mwenyewe, liruhusu likuguse kwa undani.
- Tafakari mara tena unaposoma  sehemu hiyo kwa mara ya pili. Zingatia ni mawazo gani, na hisia zipi na tafakari zipi zinazojitokeza ndani yako. Kupitia kwa maandiko Mungu anaweza kuwa anakutaka ufanye nini?

Ruhusu uwe na muda kiasi wa  shughuli hii, ili kila mmoja aweze kutafakari na kuandika. Malizia kwa maombi.

## VIFUNGU VYA BIBLIA KWA UBUNIFU – KUSOMWA NA WATOTO NA VIJANA MBALIMBALI

**Mwanzo 1:26-31; Mwanzo 2:16-17; Mwanzo 3:4-5; Warumi 5:12,15; Wagalatia 5:1; Isaya 43:1**

**Msomaji wa 1:** Mungu alisema: Natumfanye mtu kwa mfano wetu,
**Msomaji wa 2:** ili aidhihirishe hali yetu.
**Msomaji wa 3:** Mungu akaumba mtu kwa mfano wake, kwa mfano wa Mungu alimwumba, mwanaume na mwanamke.
**Wote:** Na Mungu akawabariki,
**Msomaji wa 1:** Mungu akaona kila kitu alichokifanya;
**Msomaji wa 2:** na tazama, ni chema sana,
**Wote:** chema sana!
**Msomaji wa 3:** Bwana Mungu akamwagiza huyo mtu akisema:
**Msomaji wa 1:** Matunda ya kila mti wa bustani waweza kula,
**Msomaji wa 2:** walakini matunda ya mti wa ujuzi wa mema na mabaya usile, (unaweza kuonyesha kidole kwa picha ya mti)
**Msomaji wa 3:** kwa maana siku utakapokula matunda ya mti huo utakufa hakika.
**Wote:** Utakufa hakika!
**Msomaji wa 1:** Hakika hamtakufa, mtakuwa kama Mungu, mkijua mema na mabaya.
**Msomaji wa 2:** Mtakufa!
**Wote:** (Mmesimama kwa ukimya)
**Msomaji wa 3:** Uko wapi?
**Msomaji wa 1:** Umefanya nini?
**Msomaji wa 2:** Kwa mtu mmoja, dhambi,
**Msomaji wa 3:** kwa dhambi, mauti.
**Msomaji wa 1:** Kwa mtu mmoja, maisha,
**Msomaji wa 2:** maisha huru, maisha bora makamilifu.
**Wote:** Yesu Kristo, mwana wa Mungu.
**Msomaji wa 2:** Sasa sisi tu huru.
**Wote:** Huru!
**Msomaji wa 3:** Hakuna tena utumwa.
**Wote:** Huru!
**Msomaji wa 1:** Sisi sasa ni watoto wa Mungu.
**Msomaji wa 2:** Kwa kuwa nimekukomboa wewe.
**Msomaji wa 3:** Nimekuita kwa jina lako.
**Wote:** Wewe ni wangu.

***Wimbo***

Chagua wimbo kutoka kwenye orodha iliyopendekezwa au wimbo wowote unaofikiria ni sahihi kwa wakati wako.

# SHUGHULI YA VIOO – SHUGHULI YA USHUHUDA*



**Nyenzo:**

- Kioo
- Karatasi
- Penseli

*Kabla ya mkutano, waombe kila mmoja aje na kioo kidogo. Wape karatasi na penseli. Kama mkutano unafanyika kimtandao, waombe waviandae vitu hivi mapema.*

*Waalike wasimame mbele ya kioo.*

*Sema: Asubuhi watu wengi huenda kwenye kioo ili wajitizame waone kama wanaonekana vizuri au hapana. Sitawaomba mfanye hivyo, lakini nitawaomba mwende mbele ya kioo na karatasi na penseli, jitizame kwa sekunde 60, jichambue kwa uaminifu, gawa karatasi yako sehemu nne na uandike majibu yako ya maswali yafuatayo..*

| | |
|---|---|
| Unaona uzuri gani katika tabia za mtu anayeonekana kwenye kioo? | Unaona nini ambacho sio kizuri sana katika tabia za mtu anayeonekana kwenye kioo? |
| Mungu huona nini anapomtizama mtu anayeonekana kwenye kioo? | Ombea mambo uliyoyaandika chini katika hizo sehemu tatu. Mwombee mtu anayeonekana kwenye kioo. |

Wape muda wa kushuhudia kuhusu maombi na maamuzi yaliyofanywa na kila mmoja.

***Wimbo***

Chagua wimbo kutoka kwenye orodha iliyopendekezwa au wimbo wowote unaofikiria ni sahihi kwa wakati wako.

## UJUMBE SEHEMU YA 1– MAISHA MARA MOJA

### UTANGULIZI

Hadithi hii inakuhusu wewe na mimi. Ni juu ya watu wanaofahamu nini maana ya kuvutia. Ni hadithi juu ya watu wanaotambua kukataliwa maana yake nini. Ni juu ya watu wenye ndoto. Ni juu ya watu wenye maono. Ni juu ya watu ambao wako chini na watu wanaonyanyuka juu.

Hadithi hii ni juu yako wewe, mimi na Yusufu, mtu mmoja wa ajabu katika kitabu cha Mwanzo. Ulimwengu wake ulichanganya kupendwa na baba yake lakini kuchukiwa na kufanyiwa wivu na ndugu zake. Aliachwa na ndugu zake katika nchi yake, lakini akakaribishwa na mtu mgeni kwake katika nchi ya ugenini. Aliuzwa kama mtumwa na akawa mfungwa, na akawekwa huru atawale nchi. Na katika matukio yote haya makubwa, hakubadilika. Hilo liliwezekana vipi? Tunakwenda kuligundua hili pamoja!

## MAISHA MARA MOJA

Sio bahati mbaya kwamba Biblia inaanza na hadithi ya uumbaji. Bila shaka, sisi kama binadamu tunataka kufahamu tunakotokea. Chimbuko letu ni lipi? Mwanzo inatudhihirishia wazi kwamba tunatokana na Mungu. Yeye ndiye sababu ya sisi kuwepo. Naye hufurahia uwepo wetu! Amejaa sifa juu ya uumbaji wetu.

Biblia katika kitabu cha Mwanzo inatueleza juu ya mawazo na hitimisho la Mungu juu ya uumbaji wake mkamilifu, na analielezea hilo kwa maneno rahisi:

***‘Mungu akaona kila kitu alichokifanya , na tazama ni chema sana.’***

**(Mwanzo 1:31)**

Kwa hiyo, wewe ni nani? Wewe ni kiumbe uliyeumbwa na Mungu. Wewe ni kiumbe asilia sio nakala, toleo lake! Tunapojitizama, tunachoweza kufanya ni kujishangaa tuu. Sisi ni wa kipekee! Sote tunapendwa na tunajulikana na Mungu. Kwa hiyo, kila kimoja ni chema, sahihi? Kwa kweli sivyo sana. Hebu mtizame Yusufu.

Yusufu alikuwa mtoto wa kiume mpendwa wa Yakobo. Alipendwa sana na baba yake kiasi kwamba baba yake alimnunulia koti maalum. Lakini hili lilikuja na gharama yake: ndugu zake walimchukia. Na juu ya hilo, Yusufu aliwashirikisha ndoto zake maalum. Kwa hiyo ndugu zake walimchukia hata zaidi na kwa mzaha wakamwita ‘bwana wa ndoto’ (Mwanzo 37:19).

Sijui kama Yusufu alikuwa anafahamu mienendo hii. Na je alifahamu nguvu iliyokuwa katika maono yake? Ilikuwa moja ya nguvu zake, lakini iliweza kuwa udhaifu wake vile vile, kama alikuwa hazungumzii tuu juu ya ndoto zake, lakini alikuwa anajivuna na kuwa mwenye kiburi. Alifahamu ilimaanisha nini kupendwa na kuchukiwa kwa wakati huo huo; kujisikia wewe ni wa muhimu na kwa wakati huo huo umeachwa. Mchanganyiko wa mambo makubwa na Yusufu aliyapitia yote.

Sijui dunia yako ikoje. Unajisikia unapendwa? Unajisikia kuwa wa kipekee? Unajisikia unachukiwa? Unajisikia kutengwa?

Tunakualika usome ushuhuda ufuatao:

*Ninavyojisikia na kudhihirisha tabia yangu hubadilika mara kwa mara. Wakati fulani na kuwa rafiki na hutabasamu, na wakati mwingine huwa hata sijifahamu mimi mwenyewe. Huwatendea vibaya watu wa familia yangu, kisha nagundua kosa na kujisikia vibaya. Lakini naona kama hawanielewi. Wakati fulani huwa hata sijielewi mimi mwenyewe.*

*Ndiyo maana napenda kuwa peke yangu nikichezea kompyuta au simu yangu ya mkononi, huko mambo ni rahisi. Kama nikishinda, nashinda, na kama nikishindwa, nashindwa. Hakuna linalotokea nami huanza upya. Hata hivyo mimi mzuri sana kwenye kucheza, mimi hufanya vema na vema zaidi, mimi huenda masafa na kupata alama nzuri, mimi hununua silaha nzuri zaidi na huwashirikisha wengine maisha yangu kwenye mtandao. Mimi huwa na furaha. Hunifanya nijisikie vizuri na nisijisikie mpweke, mwenye hasira au aliyehukumiwa.*

*Ninapokuwa nacheza sifikirii jambo jingine lolote. Kwa kweli sipendi kufikiri. Ninapofikiri, nakumbuka kwamba nyumbani hakuna fedha na hilo huwa zito; kwamba wazazi wangu huwa wanagombana tuu; na kwamba haijalishi kwamba mimi nipo hapa peke yangu kwa masaa au hata kwa siku zote; na kwamba sina marafiki wanaonifahamu mimi ni nani, nafikiri nini, napenda nini, nina ndoto zipi, au naogopa nini.*

*Sipendi kufikiria na kwenda kujifunza nini na nitafanya nini siku zangu za usoni. Yote kwa kweli hayana uhakika. Sipendi kufikiria kwamba sina rafiki wa kike na kwa mwendo ninaokwenda nao sitampata hata mmoja. Sipendi kuyafikiria haya kwani hunifanya niwe mpweke, nijisikie kuogopa, mwenye hasira na huzuni.*

*Kama ungeniuliza kama napenda kuwa na marafiki, tuende nje tuzungumze, tucheze michezo, tupande milimani au twende ufukweni, twende kwenye kambi, tukatembee, twende sinema, kwa kweli ningependa sana kufanya haya. Lakini kuna mdudu ndiyo maana ni bora kukaa nyumbani tu. Pia ni kwamba siwajui watu wengi*

*niwashe kamera kwenye darasa la mtandaoni ili tuonane. Sipendi nionekane.*

Janga la UVIKO lilituletea changamoto nyingi. Hadithi yako juu ya miaka iliyopita inaweza kuwa hadithi ya nyakati za giza. Nyakati ambazo ulijisikia kutengwa na ukawa mpweke. Kama vile birikani na gerezani kwenye hadithi ya Yusufu. Hatusomi lolote linaloonyesha Yusufu alikata tamaa. Je, inaweza kuwa aliamini kwamba birika na gereza haikuwa mwisho wa hadithi yake? Inaweza kuwa hakupoteza uwezo wake wa kuota ndoto na kuwa na matumaini?

Nakupa changamoto ya maswali haya:

- Unajisikia unapendwa na nani?
- Unajisikia vizuri vya kutosha?
- Unaamini nini kuhusu hadithi yako?
- 

**Nyimbo zinazopendekezwa:**

- **Spanish**
  - 'Dios de la Creación'
  - 'Dios de Maravillas'
  - 'Dios Incomparable'

- **English (Kiingereza)**
  - 'Creation Song' – Wimbo wa uumbaji
  - 'God of Wonders' – Mungu wa maajabu

- **Songs from the movie Joseph, King of Dreams such as (Nyimbo kutoka kwenye sinema ya Yusufu, Mfalme wa Ndoto):**
  - 'More than you Take'
  - 'Miracle Child'

- **Other songs and videos (Nyimbo zingine na video)**
  - 'Known'
  - 'You Say'
  - 'This is Amazing Grace'
  - 'I Can Only Imagine'
  - 'You Will be Found'

## Jumamosi • Dunia

Kutumia siku hii kuendesha shughuli katika jamii, kama ikiwezekana, kutegemea hali ya hili janga katika mji wako. Kusudi ni kuungana na ulimwengu unaotuzunguka, hivyo jiunge wa watu katika jamii yako, kwa kutumia uwezo, ujuzi, karama na ufundi wa watoto na vijana.

Kama unaweza kufanya shughuli nje ya nyumba yako, watake vijana wafanye shughuli kama:

- Flash mobs zenye koleografia zinazoshinda.
- Michezo ya nguvu kama michezo ya maswali na chemsha bongo. (Jaribu kahoot kwenye https://kahoot.it/ na utengeneze maswali yako mwenyewe, ingiza video na picha.)
- Mashindano.
- Jumbe kwenye taa za trafiki (kama mabango ya kutengeneza wenyewe au hata ‘kutembea na msalaba na muziki’).
- Karatasi za kugawa (zilizotengenezwa na wenyewe) vitafunwa au keki kwa majirani zikiwa na kifungu cha Biblia kwenye kadi.
- Kituo cha maombi, mahali watu wanaweza kwenda wakaombewe au kusanya mahitaji yao ya maombi yaliyoandikwa kwenye kadi na uzigawe kwa waumini ili wajitoe kuwaombea hao watu.

Kama shughuli za nje ya nyumba sio rahisi kufanyika, watake watoto na vijana watengeneze mabango yenye vifungu vya Biblia na wayabandike kwenye madirisha yao.

Vifungu hivi hivi vinaweza kutengenezewa picha na ziingizwe kwenye mtandao wa jamii zikiwa na hashtag #TSA1life1world1God

Kumalizia shughuli hizi, fanya mkutano wa kufunga.

## Sugerencias para el programa

***Wimbo wa kiini***

Umeniumba kwa mikono yako, Bwana.
Nina maisha tele kupitia kwa pendo lako.
Siishi tena katika minyororo ya dhambi na mauti.
Waniweka huru, Bwana, Waniweka huru, Bwana,

Kuna uhuru katika wewe tuu.
Nina uzima wa milele katika wewe.

Twasherehekea na kucheza kulitukuza jina lako
Kwa ajili ya pendo lako la ajabu.
Hata katika dhoruba nitakuimbia wewe
Kwa ajili ya pendo lako la ajabu, Yesu!

Ninapojisikia kutengwa na kuachwa,
mikono yako ya upendo hunizunguka, Ninalindwa.
Nakufahamu wewe Mungu wangu, utanipenda siku zote
nami nakupenda, nami nakupenda.

## UTANGULIZI WA KIINI – MNENAJI WA 2 – DUNIA MOJA – NAWEZA KULETA TOFAUTI GANI?

Habari, ni mimi tena.  Sasa nina umri wa miaka 30.

Ndoto zangu mwenyewe zilinileta Misri kwa njia ya ajabu sana. Nimesafirishwa! Waishmaeli fulani walininunua kwa vipande 20 vya fedha. Wakaja na kuniuza kwa mtu huyu anayeitwa Potifa, mmoja wa wafanyakazi wa Farao.

Nilimfanyia kazi nikafanya vizuri sana. Halafu akawepo mke wake...Kila siku mwanamke huyu aliniingiza kwenye shida. Alining'ang'ania! Akiniambia mimi mzuri sana... Akiniomba niungane naye kwenye matembezi yake...Mambo ya namna hiyo. Sikujisikia vizuri. Siku moja akanishitaki eti nimemtongoza. Lakini mimi sikufanya chochote! Bwana wangu hata hivyo hakuniamini. Alikasirika sana akanitupa gerezani. Mahali pa giza sana. Nilikasirika, nikasononeka, nikajawa na hofu; yote hayo. Ingawa, nilitaka sana kung'ang'ania ndoto zangu. Huu usingeweza kuwa mwisho wangu!

Kwa namna fulani, nilikuja nikatoka kwenye sehemu hiyo ya giza. Walinipenda wakanifanya niwe msimamizi wa wafungwa.

Wafungwa wengine wawili walipoota ndoto, niliweza kuwaelezea maana ya ndoto hizo. Hilo lilinileta kwa Farao, yeye mwenyewe aliota ndoto nami niliweza kuwaelezea ndoto hizo zilikuwa na maana gani. Zilionyesha yatakayotokea siku zijazo. Tutakuwa na miaka saba ya chakula kingi kisha miaka saba ya njaa. Kwa hiyo, Farao akaniweka mimi nisimamie nchi nzima ya Misri ili kuwaokoa watu na janga hilo la njaa.

Ukweli, bado nimechanganyikiwa kuhusu badiliko hili. Kutoka shimoni (birikani) hadi Ikulu... Unaweza kuamini hilo? Nilijitoa kikamilifu, Farao akagundua uwezo wangu akanipa nafasi ili niwatumikie wananchi. Ni hisia ya ajabu: najua ninajambo la kuchangia. Sio ndoto!

***Wimbo***

Chagua wimbo kutoka kwenye orodha iliyopendekezwa au wimbo wowote unaofikiria ni sahihi kwa wakati wako.

# A SHUGHULI ZA KIKUNDI: GUNDUA THAMANI YAKO NA KARAMA ZAKO

Unda mchezo wa ‘ Gundua thamani na talanta. ‘ Huenda pana mchezo au chemsha bongo katika lugha yako unayoweza kuitumia. Unaweza vile vile ukatumia maswali yaliyoko hapa chini. Gawa nakala iliyochapishwa ya maswali kwa kila mmoja na waombe wayajibu. Kuna ziada kwa ajili ya majibu ya ziada.



1. **Mimi hufurahia nini zaidi?**

___

___

___

2. **Ni mambo gani mimi huyafanya vizuri?**

___

___

___

3. **Ni mambo gani niyafanyayo huwafanya watu wengine wafurahi?**

___

___

___

4. **Kutokana na wengine nini ni sifa na karama zangu kulingana na wengine? Waulize!**

Wape kila mmoja muda wa kujibu maswali haya wao wenyewe. Vile vile wape mda kuzungumza na wenzao juu ya swali la nne.

Baada ya hayo, njoni pamoja kama kikundi na mzungumze kuhusu mahitaji kwenye jamii. Wameona mahitaji gani? Ni watu gani walio katika mazingira magumu katika jamii? Chukua karatasi kubwa  (A3 au A2) na andika kila kitu chini au tengeneza waraka wa mtandaoni (https://www.wordclouds.com).

Jitahidi kugundua mahitaji makuu katika jamii yako.

Kisha washirikishe wengine picha hii na maneno ya Aristotle:

> “Pale mahitaji ya dunia na karama zako zinapokutania, hapo ndipo wito wako ulipo”
>
> Aristoteli

Funga na swali: unaweza kukabiliana vipi na mahitaji ya jamii kwa kutumia sifa na karama zako? Waache watu waandike majibu yao kwenye taarifa ya awali na waache waiweke kwenye karatasi ya mahitaji.

## UJUMBE SEHEMU YA 2 – DUNIA MOJA – NAWEZA KULETA TOFAUTI GANI?

Unajua kifungu maarufu sana katika Biblia ni kipi? Jaribu! Ni Yohana 3:16

***'Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.'***

**(Yohana 3:16)**

Mungu anaupenda ulimwengu! Na Mungu anaupenda sana, hata akajitoa yeye mwenyewe katika Yesu Kristo kwa ajili ya huo ulimwengu. Ulimwengu wa miaka 2000 iliyopita na ulimwengu wa hivi sasa.

Ulimwengu wa Yusufu ulikuwa tofauti, lakini kwa wakati ule ule, mambo mengi yalikuwa kama yalivyo katika siku zetu hizi. Walikuwepo watu waliomtia moyo na kumpenda, kama alivyofanya baba yake. Na walikuwepo watu waliomvunja moyo na waliomkataa, kama walivyofanya ndugu zake. Walikuwepo watu waliomwamini na wakampa majukumu, kama alivyofanya Potifa na Farao, na hawa walikuwa watu waliotaka kumtumia kwa manufaa yao, kama vile wafanya biashara Wamidiani na mke wa Potifa.

Yusufu angeweza kwa urahisi kukatishwa tamaa kwa wivu na kutendewa mabaya na ndugu zake. Angeweza kukatishwa tamaa alipopelekwa gerezani akiwa hana kosa. Ingekuwa rahisi namna gani kusahau ndoto zake, upendo wa baba yake, karama zake za kipekee? Lakini hakusahau hayo yote. Na kwa hiyo, wakati ulipowadia, aliweza kuleta tofauti! Aliweza kumwokoa mfanyakazi muhimu sana wa Farao alipokuwa gerezani. Aliweza kuitafsiri ndoto ya Farao:

***'Ndivyo nilivyomwambia Farao, ya kwamba Mungu amemwonyesha Farao atakayoyafanya hivi karibu. Tazama, miaka saba ya shibe inakuja, katika nchi yote ya Misri. Kisha kutakuja miaka saba ya njaa baada yake, na shibe ile yote itasahauliwa katika nchi ya Misri, na njaa itaiharibu nchi.'***

**(Mwanzo 41:28-30)**

Na aliweza kuwaokoa watu wengi kutokana na njaa:

***'Njaa ikawa katika dunia yote pia. Yusufu akazifungua ghala zote, akawauzia Wamisri. Njaa ikawa nzito katika nchi ya Misri. Watu wa nchi zote wakaja Misri kwa Yusufu; ili wanunue nafaka; kwa sababu njaa imekuwa nzito katika dunia yote.'***

**(Mwanzo 41:56-57)**

Roho wa Mungu alifanya kazi kupitia kwa Yusufu wakati wote. Roho huyu alimweka huru kutokana na maisha chini ya mawingu meusi. Ni kama nguvu mpya ilimwandaa na kumvika aweze kuleta tofauti kubwa duniani! Inaweza kuwa Yusufu alielewa nini maana ya kukataliwa na kuokolewa, kufungwa gerezani na kuachiwa huru? Inawezekana alifahamu Mungu alikuwa nyuma ya matukio yote haya na kwa hiyo akaweza kuendelea kuishi katika maisha haya mapya, yenye nafasi na yaliyo huru? Hii inatukumbusha aliyoyaandika Paulo:

***'Katika uungwana huo Kristo alituandika huru; kwa hiyo simameni, wala msinaswe tena chini ya kongwa la utumwa.'***

**(Wagalatia 5:1)**

*Inawezekana Yusufu alitambua ameokolewa (kutokana na utumwa), ili awaokoe wengine (kutoka kwenye utumwa)?*

Nakupa changamoto kwa maswali yafuatayo:

- Mtazamo wako ulikuwa upi ulipokabiliana na nyakati za giza nene miezi iliyopita?

*Tunaishi katika dunia moja, lakini kila mmoja wetu anaishi mahali tofauti katika dunia hii. Unaweza kuusikia uzito wa kutaka kukubalika na wengine. Unaweza kuusikia msukumo toka kwa wenye rika moja na wewe, shuleni au chuoni. Unaweza kuusikia uzito wa kutafuta kazi au kuitunza kazi. Hauko peke yako! Hebu watizame wengine na mtizame Yusufu. Mruhusu Roho wa Mungu akupe nguvu za ndani unazohitaji.*

- Unaweza kuchangia nini kwa dunia hii?

*Nafasi zetu za kutoa mchango wetu kwa dunia hutegemea tunaishi wapi na shauku ya mtu binafsi, karama zake, ujuzi wake, mtandao wake na uzoefu wake. Ndoto yako ni ipi? Nguvu yako ni ipi? Shauku yako ni ipi? Mungu amekupa haya kwa kusudi: ili uwe sehemu ya hadithi ya Mungu ya kuiokoa dunia yenye mahitaji. Kwa hiyo, jitokeze na ufanye jambo fulani, kama William Booth alivyopenda kusema! Sisi ni watu huru katika Yesu nasi tumeitwa kuwatumikia wengine kwa kila tulichonacho, ili nao wawe na maisha hayo huru na yenye nafasi, mahali ambapo Roho wa Mungu anatolewa kama nguvu mpya kila siku.*

### Mapendekezo ya nyimbo

- **Spanish**
  - 'Necesitan de Cristo'
  - 'Solo Dios Puede Salvar'
- **English (Kiingereza)**
  - 'They Need Christ'
  - 'Mighty to Save'
- **Songs from the movie Joseph, King of Dreams such as: (Nyimbo toka kwenye sinema ya Yusufu Mfalme wa Ndoto kama:**
  - 'More than You Take' - (Zaidi ya unachukua)
  - 'Miracle Child' - (Mtoto wa miujiza)
- **Other songs and videos (Nyimbo zingine na video)**
  - 'Shackles' - (Pingu)
  - 'You Will be Found' - (Utapatikana)
  - 'Freedom' – (Uhuru)

z

## Pendekezo la ratiba

***Wimbo wa Kiini***

Umeniumba kwa mikono yako, Bwana.
Nina maisha tele kupitia kwa pendo lako.
Siishi tena katika minyororo ya dhambi na mauti.
Waniweka huru, Bwana, Waniweka huru, Bwana,

Kuna uhuru katika wewe tuu.
Nina uzima wa milele katika wewe.

Twasherehekea na kucheza kulitukuza jina lako
Kwa ajili ya pendo lako la ajabu.
Hata katika dhoruba nitakuimbia wewe
Kwa ajili ya pendo lako la ajabu, Yesu!

Ninapojisikia kutengwa na kuachwa,
mikono yako ya upendo hunizunguka, Ninalindwa.
Nakufahamu wewe Mungu wangu, utanipenda siku zote
nami nakupenda, nami nakupenda.

## MNENAJI WA 3 – MUNGU MMOJA – WA WOTE

Habari! Ni mimi mara tena.  Sasa umri wangu ni miaka 40.

[Akiwa na furaha] Unajua kilichotokea leo? Nilikutana na ndugu zangu, mara tena! Walikuja Misri kutafuta chakula, kwa sababu sisi tuna chakula kingi katika ghala zetu nao wana njaa, huko Kanani. Kweli, unaweza kufikiria nilivyojisikia? Sijawahi kujisikia kuchanganyikiwa na hisia namna hii na sikuweza kujizuia kutoa machozi.

Kwa hiyo, leo ndugu zangu walisimama mbele yangu. Sikuwa tena kijana mdogo kwao. Hata wao. Sote tulikuwa wanaume. Niliwatambua mara moja, ingawa wamekonda na walionekana wamechoka. Lakini hawakunitambua mimi. Hivyo niliwataka wanisogelee. Taratibu walinisogelea. Nilimwona Ruben anachechemea. Walikuwa karibu sana, niliweza kuwatizama machoni. Niliona kukata tamaa kwao. Karibu nionje njaa yao.

Ghafla nikang'amua kitu. Mimi ndugu yao. Tuna baba mmoja. Damu yake inatembea katika mishipa yetu. Inashangaza kwamba sikujisikia kuwakasirikia, wivu au kulipiza kisasi. Nilichotaka kufanya ni kuwakumbatia na kuwashikilia tu. Niwe sehemu ya familia yetu mara tena.  Nilitambua vile vile kwamba Mungu yuko nyuma ya mambo haya yote. Mimi ni sehemu ya mpango mkubwa. Shimoni (birikani), ile safari, nyumbani kwa Potifa, gerezani... Mungu alikuwa pamoja nami wakati wote. Na Mungu alinituma mbele ya familia yangu, ili niweze kuyaokoa maisha yao kwa njia moja ya ajabu.

Mungu alikuwa hajaniacha. Ilikuwa zaidi ya ndoto kwa namna fulani!

## SHUGHULI YA MIKONO YA MAOMBI (MUNGU MMOJA)



**Nyenzo:**

- Kitambaa cheupe au cardboard
- Rahisi kusafisha, rangi iliyo nyepesi kukauka
- Kalamu kubwa
- Vifutio au maji na karatasi - kuosha na kupangusia mikono

1. Wanapowasili kwenye mkutano, watake washiriki waweke mchoro wa viganja vya mikono yao kwenye ubao wa matangazo au kwenye kitambaa cheupe. Tayarisha mapema rangi ambayo washiriki watatumia kuwekea mchoro wa viganja vya mikono yao. Toa muda rangi ikauke.
2. Wakati wa maombi, watake washiriki waandike maombi kwenye mchoro wa kiganja cha mkono walichotengeneza, kufuatana na kiini cha Maisha mara Moja, Dunia Moja, Mungu Mmoja
3. Maombi haya yafanywe kwa pamoja. (Toa nafasi ya kuacha michoro ya viganja vya mikono ibakie haijulikani ni ya nani labda tuu wao wenyewe watake kujitangaza.)

***Wimbo***

Chagua wimbo kutoka kwenye orodha iliyopendekezwa au wimbo wowote unaofikiria ni sahihi kwa wakati wako.

## VIFUNGU VYA BIBLIA KWA UBUNIFU – KUSOMWA NA WATOTO NA VIJANA MBALIMBALI

**Mwanzo 1:26-31; Mwanzo 2:16-17; Mwanzo 3:4-5; Warumi 5:12,15; Wagalatia 5:1; Isaya 43:1**

**Msomaji wa 1:** Mungu alisema: Natumfanye mtu kwa mfano wetu,
**Msomaji wa 2:** ili aidhihirishe hali yetu.
**Msomaji wa 3:** Mungu akaumba mtu kwa mfano wake, kwa mfano wa Mungu alimwumba, mwanaume na mwanamke.
**Wote:** Na Mungu akawabariki,
**Msomaji wa 1:** Mungu akaona kila kitu alichokifanya;
**Msomaji wa 2:** na tazama, ni chema sana,
**Wote:** chema sana!
**Msomaji wa 3:** Bwana Mungu akamwagiza huyo mtu akisema:
**Msomaji wa 1:** Matunda ya kila mti wa bustani waweza kula,
**Msomaji wa 2:** walakini matunda ya mti wa ujuzi wa mema na mabaya usile, (unaweza kuonyesha kidole kwa picha ya mti)
**Msomaji wa 3:** kwa maana siku utakapokula matunda ya mti huo utakufa hakika.
**Wote:** Utakufa hakika!
**Msomaji wa 1:** Hakika hamtakufa, mtakuwa kama Mungu, mkijua mema na mabaya.
**Msomaji wa 2:** Mtakufa!
**Wote:** (Mmesimama kwa ukimya)
**Msomaji wa 3:** Uko wapi?
**Msomaji wa 1:** Umefanya nini?
**Msomaji wa 2:** Kwa mtu mmoja, dhambi,
**Msomaji wa 3:** kwa dhambi, mauti.
**Msomaji wa 1:** Kwa mtu mmoja, maisha,
**Msomaji wa 2:** maisha huru, maisha bora makamilifu.
**Wote:** Yesu Kristo, mwana wa Mungu.
**Msomaji wa 2:** Sasa sisi tu huru.
**Wote:** Huru!
**Msomaji wa 3:** Hakuna tena utumwa.
**Wote:** Huru!
**Msomaji wa 1:** Sisi sasa ni watoto wa Mungu.
**Msomaji wa 2:** Kwa kuwa nimekukomboa wewe.
**Msomaji wa 3:** Nimekuita kwa jina lako.
**Wote:** Wewe ni wangu.

MAISHA MARA MOJA • DUNIA MOJA • MUNGU MMOJA •

## SHUHUDA NA MICHANGO YA UBUNIFU

Nafasi hii inatoa fursa ya kushirikishana yaliyofanyika siku zilizopita. Uwe huru kuwa mbunifu uwezavyo.

## MATANGAZO NA SADAKA

## UJUMBE SEHEMU YA 3 – MUNGU MMOJA

Hebu nikuulize swali: umeona alama za barabarani ngapi juma hili? Kwa kweli, tunazihitaji hizo alama ili kutukumbusha tunatakiwa kufanya nini. Biblia imejaa 'alama' zinazotusaidia kukumbuka namna gani tufikirie, namna gani tuamini na tufanye. Waisraeli walikumbushana kwa maneno rahisi kwamba yupo Mungu mmoja, kama katika Kumbukumbu la Torati:

***'Sikiza, Ee Israeli; Bwana, Mungu wetu, Bwana ndiye mmoja!'***

**(Kumbukumbu la Torati 6:4)**

Mungu mmoja kwa ajili ya Dunia moja. Waisraeli walilazimika kukumbushana kuhusu Mungu mmoja hata sisi tunatakiwa kufanya hivyo. Inakuwa kama haiwezekani kutambua kwamba Mungu wa Israeli ni Mungu wa dunia yote. Kupitia kwa Roho wake Mungu yumo katika maisha mbalimbali ya watu na mahali tofauti tofauti. Hilo si la kustaajabisha?

Yusufu aliishi sehemu mbalimbali. Alizaliwa Kanani akaletwa Misri. Misri alifanya kazi katika nyumba ya Potifa. Angalia vifungu hivi:

***'Basi Yusufu akaletwa mpaka Misri; naye Potifa, akida wa Farao, mkuu wa askari, mtu wa Misri, akamnunua mkononi mwa hao Waishmaeli waliomleta huko. Bwana akawa pamoja na Yusufu, naye akasitawi, naye alikuwa katika nyumba ya bwana wake, yule Mmisri.'***

**(Mwanzo 39:1-2)**

Kwa bahati mbaya, Yusufu kimakosa aliishia gerezani kwa sababu ya mke wa Potifa, aliyemshitaki eti alimtongoza.

***'Bwana wake akamtwaa Yusufu, akamtia gerezani, mahali walipofungwa wafungwa wa mfalme, naye akawamo humo gerezani. Lakini Bwana akawa pamoja na Yusufu, akamfadhili, akampa kibali machoni pa mkuu wa gereza.***

**(Mwanzo 39:20-21)**

Baada ya miaka miwili Yusufu alitolewa gerezani akaanza kufanya kazi kwa Farao. Ilikuwa tuu wakati Yusufu alipokutana na ndugu zake tena, ndipo alipofahamu kwamba Mungu mmoja yupo pamoja naye kila mahali:

***'Yusufu akawaambia ndugu zake, mimi ndimi Yusufu, baba yangu angali hai bado? Wala ndugu zake hawakuweza kumjibu, maana waliingiwa na hofu mbele yake. Yusufu akawaambia ndugu zake, karibuni kwangu, basi wakakaribia. Akasema mimi ni Yusufu, ndugu yenu, ambaye mliniuza kwenda Misri. Basi sasa msuhuzunike, wala msiudhike nafsi zenu, kwa kuniuza huku, maana Mungu alinipeleka mbele yenu kuhifadhi maisha ya watu.'***

**(Mwanzo 45:3-5)**

Kila alikokwenda Yusufu, wema wa Mungu ulikuwa pamoja naye, kupitia kwa watu wengine kama baba yake, Potifa, na Farao. Na kwa kustaajabisha zaidi, Mungu alikuwepo vile vile wakati Yusufu alipotupwa shimoni (birikani) na ndugu zake na akauzwa kwa Waishmaeli. Huyu Mungu mmoja yupo kila mahali: tayari kwa kila mmoja. Mungu mmoja ambaye kila mara anatufikia akibadilisha yote kuwa mema zaidi. Ukitizama nyuma, Yusufu aliona kusudi la safari yake na maisha yake. Aliitwa ili kuiokoa familia yake! Na jambo jingine lilitokea: aliwasamehe ndugu zake na akawaweka huru wasijisikie wana hatia. Sasa kila mmoja wao aliweza kuishi maisha yaliyo huru na yenye nafasi! Naweza kusema ni ukombozi mara mbili.

Ni zaidi ya ufahamu wetu kwamba huyu Mungu mmoja ni Mungu wa wote. Yeye ndiye Mungu mmoja mkuu, anayejiruhusu awepo kwa ajili ya kila mmoja: wachanga, wazee, matajiri, masikini, wakubwa au wadogo. Yeye ni Mungu wa wale uwapendao na Mungu wa wale usiowapenda sana.

Wakati fulani unamwona Mungu tuu wakati unapotizama nyuma katika maisha yako. Lakini unaweza kumuona Mungu vile vile katika maisha yako ya kila siku hapa na sasa. Nakupa changamoto uyafikirie maswali yafuatayo:

Ni watu gani hunionyesha wema wa Mungu?
Lini na wapi mimi hujisikia kuwa karibu sana na Mungu?

Wewe ni kiumbe asilia wa uumbaji wa Mungu. Umechaguliwa. Umewekwa huru kuishi maisha yenye nafasi. Umeitwa ili kuwashirikisha wengine ndoto zako, karama zako, ili kila mmoja awe na maisha yale yale yaliyo huru, yenye nafasi na wamfahamu Mungu kama baba yao.

Wazo: wape watu changamoto kwa ajili ya maisha yao ya kila siku.
Watafikiria nini, watasema nini na watafanya nini kwa tofauti?
Wanaweza kujitolea namna gani kwa Mungu na kwa wengine?

Siishi tena katika minyororo ya dhambi na mauti.
Waniweka huru, Bwana, Waniweka huru, Bwana,

Kuna uhuru katika wewe tuu.
Nina uzima wa milele katika wewe.

Twasherehekea na kucheza kulitukuza jina lako
Kwa ajili ya pendo lako la ajabu.
Hata katika dhoruba nitakuimbia wewe
Kwa ajili ya pendo lako la ajabu, Yesu!

Ninapojisikia kutengwa na kuachwa,
mikono yako ya upendo hunizunguka, Ninalindwa.
Nakufahamu wewe Mungu wangu, utanipenda siku zote
nami nakupenda, nami nakupenda.

## Mapendekezo ya nyimbo

- **Spanish**
  - 'Dios Poderoso'
  - 'Dios viene a mi'
  - 'El poder de Tu amor'
- **English (Kiingereza)**
  - 'Almighty Maker' – (Muumba mkuu)
  - 'When God Comes Near '- (Mungu anapokija karibu)
  - 'The Power of Your Love' - (Nguvu ya pendo lako)
- **Other songs and videos (Nyimbo nyingine na video)**
  - 'I See You in Everything' - (Nakuona katika kila kitu)

## IMANI HUZUNGUMZA ( TOLEO LA MAISHA MARA MOJA, DUNIA MOJA, MUNGU MMOJA)

Kwa kuongozwa na mchezo wa kadi wa Imani huzungumza *(https://sar.my/faithtalks) tulitengeneza mchezo wa kadi ili muutumie kuchezea. Unaweza kuzipata hizo kadi kwenye ukurasa wa mtandao ulipoukuta ukurasa huu. Zichapishe hizo kadi na uzigawe kwa makundi ( Maisha mara moja, Dunia Moja, Mungu Mmoja, na Mwisho). Hizo kadi zifunike uso chini kwenye meza na uwaache washiriki wachague kadi kutoka kwenye kundi linalostahili.*

Lengo ni kuanzisha mazungumzo kati ya washiriki. Kufunga mda huu wa ibada, tumia kadi za njano.

### Maswali ya kadi ya pink (Maisha mara Moja)

1. Yusufu alijisikia anapendwa na baba yake.  Unajisikia kupendwa na nani?
2. Yusufu alipokea zawadi gani maalum kutoka kwa baba yake? Taja zawadi maalum ambayo wewe umewahi kupokea.
3. Lini ulijisikia huridhiki na wewe mwenyewe?
4. Una ndoto zipi?
5. Mungu alikuumba. Anafahamu kuhusu nguvu zako na udhaifu wako na bado anakupenda. Hili lina maana gani kwako?
6. Uhusiano wako na marafiki zako ukoje? Uhusiano wako na familia yako ukoje?

### Maswali ya kadi za kijani (Dunia Moja)

1. ‘Potifa’ au ‘Farao’ wako ni nani ? (Mtu anayeona karama na uwezo wako naye hukutia moyo kuzitumia).
2. Shughuli zipi au mambo gani hukushusha moyo?
3. Unapokabiliana na matatizo, uhusiano wako na Mungu ukoje?
4. Unapokabiliana na matatizo, unamkaribia Mungu namna gani?
5. Karama au uwezo maalum wa Yusufu ni upi? Na wa kwako ni upi?
6. Tatizo la kutatua la Yusufu lilikuwa njaa. Tatizo la kutatua katika jamii yako ni lipi?

## Maswali ya kadi za Bluu (Mungu Mmoja)

1. Zipo nyakati wewe ungetamani kujificha Mungu asikuone? Zipi ni nyakati unatamani Mungu angekupata?
2. Huwa unajisikia kwamba Mungu anazungumza na wewe? Kama ndivyo, yeye hukuambia nini?
3. Umewahi kushirikishana na mwingine makosa yako? Hii ilikufanya ujisikiaje?
4. Unafikiri kwa nini Yusufu aliwasamehe ndugu zake? Unahitaji kumsamehe nani?
5. Lina na wapi wewe kujisikia uko karibu sana na Mungu?
6. Yesu ana maana gani kwako?

## Maswali ya Kadi ya Zambarau (Mwisho)

1. Nini kilikusaidia zaidi katika mazungumzo haya?
2. Nini kulikupa changamoto kubwa katika mazungumzo haya?
3. Ulijifunza nini kutoka kwa wengine katika mazungumzo haya?
4. Ulijisikiaje kwamba Mungu yupo katika mazungumzo haya?
5. Uligundua nini kukuhusu wewe mwenyewe katika mazungumzo haya?
6. Kuna jambo lolote ambalo unataka kulifanya au kulibadilisha baada ya mazungumzo haya?

## Maisha mara Moja

Yusufu alijisikia anapendwa na baba yake. Unajisikia kupendwa na nani?

## Maisha mara Moja

Yusufu alipokea zawadi gani maalum kutoka kwa baba yake? Taja zawadi maalum ambayo wewe umewahi kupokea.

## Maisha mara Moja

Lini ulijisikia huridhiki na wewe mwenyewe?

## Maisha mara Moja

Una ndoto zipi?

## Maisha mara Moja

Mungu alikuumba. Anafahamu kuhusu nguvu zako na udhaifu wako na bado anakupenda. Hili lina maana gani kwako?

## Maisha mara Moja

Uhusiano wako na marafiki zako ukoje? Uhusiano wako na familia yako ukoje?

## Dunia Moja

'Potifa' au 'Farao' wako ni nani ? (Mtu anayeona karama na uwezo wako naye hukutia moyo kuzitumia).

## Dunia Moja

Shughuli zipi au mambo gani hukushusha moyo?

## Dunia Moja

Unapokabiliana na matatizo, uhusiano wako na Mungu ukoje?

## Dunia Moja

Unapokabiliana na matatizo, unamkaribia Mungu namna gani?

## Dunia Moja

Karama au uwezo maalum wa Yusufu ni upi? Na wa kwako ni upi?

## Dunia Moja

Tatizo la kutatua la Yusufu lilikuwa njaa. Tatizo la kutatua katika jamii yako ni lipi?

## Mungu Mmoja

Zipo nyakati wewe ungetamani kujificha Mungu asikuone? Zipi ni nyakati unatamani Mungu angekupata?

## Mungu Mmoja

Huwa unajisikia kwamba Mungu anazungumza na wewe? Kama ndivyo, yeye hukuambia nini?

## Mungu Mmoja

Umewahi kushirikishana na mwingine makosa yako? Hii ilikufanya ujisikiaje?

## Mungu Mmoja

Unafikiri kwa nini Yusufu aliwasamehe ndugu zake? Unahitaji kumsamehe nani?

## Mungu Mmoja

Lina na wapi wewe kujisikia uko karibu sana na Mungu?

## Mungu Mmoja

Yesu ana maana gani kwako?

## Mwisho

Nini kilikusaidia zaidi katika mazungumzo haya?

## Mwisho

Nini kulikupa changamoto kubwa katika mazungumzo haya?

## Mwisho

Ulijifunza nini kutoka kwa wengine katika mazungumzo haya?

## Mwisho

Ulijisikiaje kwamba Mungu yupo katika mazungumzo haya?

## Mwisho

Uligundua nini kukuhusu wewe mwenyewe katika mazungumzo haya?

## Mwisho

Kuna jambo lolote ambalo unataka kulifanya au kulibadilisha baada ya mazungumzo haya?